jarida la kila mwezi

# NGURUMO ya mwandishi

TOLEO LA XXIII
AGOSTI MMXXIII




## Mimi Ninaandika, Wewe Unasoma...

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Mimi ninaandika, wewe unasoma—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Frank Masai—Uk 03

**New In Town:** KIKI na KWA SABABU NAKUPENDA**—**04

**PITIO LA VITABU**— Gamba la Nyoka (Ikisiri) 2—Uk 05

**MAKALA**— SAIKOLOJIA: Pambana na Maumivu ya Moyo—Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Nilimuua Dada Niolewe Na Shemeji — uk 08 na 09

**MIAMBA WA AFRIKA:** Samora Machel 06 — Uk 10

**Sako kwa Bako–** Anna Meleiya Mbise 'Msomaji, Mhamasishaji, Mwandishi wa Riwaya na Mshairi' 2**—**Uk 11

**RIWAYA:** Mpigambio 23—Uk12na 13

**RIWAYA—** Cronoc 7-Uk 14 na 15

**YA KALE NI DHAHABU**: — Aladini na Wezi 40 '2'- Uk 16

**HABARI/MATANGAZO**– Uk 17

**SHUBAKA LA VITABU:** Kitabu Maisha—Uk 18

**KITABU NILICHOSOMA: Iahi Ndoto Yako**— Uk 19

**MATANGAZO:** Uk 20

## TAHARIRI: Mimi naandika, wewe unasoma

Asalaam Aleikum watu wangu wa nguvu au niseme Amani iwe kwenu ninyi nyote!

Ni mwezi wa ishirini na tatu huu bado tupo hewani tukipumua kwa kujidai kabisa. Ngurumo ya Mwandishi linaendelea kukuletea habari na makala na mambo kemkem yanayowazunguka waandishi wetu wa riwaya hapa nchini. Ni mwezi ujao tu ambapo tutatimiza miaka miwili kamili ya kukupasha habari.

Mpaka sasa hatuna budi kuwashukuru sana wale ambao wanatumia jarida hili kupeperusha matangazo yao ya biashara. Hawa wamegundua siri ya matangazo ya biashara kukaa katika Jarida hili kwani mpaka sasa tumehakikisha linafika katika nchi kumi na nne 14 za sayari yetu. Basi kama wewe ulikuwa bado unasuasua, usifanye hivyo nakukaribisha ujitangaze kwa bei zetu rahisi kabisa. Tsh 10,000 kwa tangazo ka kurasa nzima na Tsh 5,000 kwa matangazo madogo. Namba zetu za simu zipo hapo chini.

Basi tangu tuachane katika toleo la ishirini na mbili, siku hizi thelathini zimekuwa na mambo mengi sana. Machache kati ya hayo ni kuwa tunaishukuru sana Radio Nuru FM ya pale Iringa kwa kushirikiana na Jamvi la Simulizi kuhakikisha kuwa burudani ya riwaya inawafikia Watanzania wengi zaidi. Kituo hiki cha redio kimetoa *air time* ya dakika 30 ambapo riwaya ya Mpigambio inapepea. Asanteni sana na tutazidi kuwa pamoja.

Lakini pia siku hizi za karibuni kwakweli anga la fasihi limekuwa la moto kwelikweli, kitabu juu ya kitabu vimeingia madukani. Kazi kwenu wasomaji. Kama waandishi kuandika wanaandika, sasa wasomaji mnafanya nini? Someni. Kitabu ambacho kimetikisa mitandao ya kijamii ni kile Kwa Sababu Nakupenda chake Frank Masai. Kitabu hiki kilichokuwa katika ndoto zake kwa miaka mingi kimeweza kuwa halisi na sasa kinasomwa nchini kote.

Pia Crarency Sanga naye katuletea KIKI, basi kwanini msomaji useme hakuna vitabu? Pata kitabu, soma, ujifunze.

Mimi ninaandika, wewe unasoma… ndiyo kaulimbiu ya jarida letu mwezi huu. Zaidi tunakuombeni msamaha kwa kuchelewa kutoa chapisho hili. Tarehe yetu ni ileile tano (5) ya kila mwezi.

Basi nikutakieni burudani njema.

**Richard Mwambe**
**CEO—Jamvi la Simulizi**

**NGURUMO YA MWANDISHI**

*©RICHARD MWAMBE*

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0628124486**
**WhatsApp: +255 766974865**

**jamvilasimulizi@gmail.com**

# MWANDISHI WETU: Frank Masai

**Leo katika safu ya Mwandishi wetu, tunakuja na sura nyingine kabisa. Majuma haya mawili yaliyopita kitabu Kwa Sababu Nakupenda kilichoandikwa na mwandishi Frank Masai, au kama anavyojiita kwa rakabu yake 'Mwandishi wa Watu' kimetikisa uwanda wa fasihi nchini.**

**Mwangwi wake ukatufikia mpaka kwenye ukurasa huu. Nasi tukaona 'isiwe tabu' tukamtafuta na kumbana kwa maswali mawili tuliyoyaona magumu lakini kumbe ni mepesi kwake.**

**Ngurumo:** Wazo la 'Kwa Sababu Nakupenda' lilitoka wapi?

**Frank: '**Kwa Sababu Nakupenda' ni wazo lililokuja baada ya kumaliza riwaya yangu nyingine ya mapenzi iliyoitwa 'Ganzi ya Moyo'. Wazo lilikuja baada ya rafiki yangu mmoja ambaye nilisoma naye shule ya msingi kisha tukakutana tena kidato cha tano na sita…

Yeye aliomba nitumie jina lake kwenye riwaya yoyote ya mapenzi huku akitaka mhusika ambaye ni yeye awe anafanya kazi kama yake *(Dereva Bajaji)*. Hapo ndipo wazo la Kwa Sababu Nakupenda liliibuka na kulifanyia kazi. Ilikuwa ni mwaka 2015 hiyo.

**Ngurumo:** Masai, watu wamekuzoea sana kwenye mastori ya *ki-action*, lakini nafikiri wanashangaa kuona ukitoa  vitabu laini kama 'Mwimbula' na sasa 'Kwa Sababu Nakupenda'… Unawaambiaje wasomaji wako juu ya hili?

**Frank:** Kwanza  wasomaji nawaambia, mie si wa *Ma-Action*. Uandishi wa *Action* niliuanza mwaka 2016 au 2017 na 'Duka la Roho'. Tena nakumbuka nilianza kuandika kwenye kundi sogozi la *WhatsApp* la Jamvi la Simulizi. Lakini kabla ya hapo mimi nilikuwa naandika mapenzi na maisha.

Riwaya yangu ya kwanza kunitambulisha iliitwa 'My Rose' ya mwaka 2014. hii ni mapenzi kabisa. Baadae ikaja 'Mawio na Machweo' ikawa ya maisha. Nikaandika 'Makay 88' nayo ni maisha na mapenzi. Nikaandika machombezo ya kutosha. Na baadae ndiyo nikaja kuandika *actions*.

Kwahiyo wasomaji wanapaswa kujua kuwa 'Mwimbula' na 'Kwa Sababu Nakupenda', nimezichagua zenyewe zitoke kwenye vitabu kwa sababu ndipo uwezo wangu ulipolalia. *Actions* naandika lakini nyumbani ni hizi riwaya za maisha na mapenzi.

Mbali na hilo, napenda kuwajuza tu, baada ya 'Kwa Sababu Nakupenda' nitawapa kitabu cha mapigano. Kwahiyo wasomaji mliodhani nimewasahau, kaeni mkao wa kula.




Huyu ni Frank Masai ambaye kwa sasa *'anakichafua'* huko katika mitandao ya kijamii.

Penda kusoma vitabu

JAMVI la SIMULIZI
www.richardmwambe.com

Faida za kusoma vitabu:

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

## NEW IN TOWN

**Kitabu: KIKI—Sanaa ya Siasa. By Crarency Sanga**

Ulianza kama mchezo wa kuigiza tu ili wapate attention waliyoitarajia,,wenyewe waliita KIKI
Wema msanii maarufu nchini Tz anazusha kifo chake siku chache kabla ya siku yake ya kuzaliwa,,hilo halikuwa tatizo.

Mapokeo ya mtandao yanakuwa makubwa ,,huenda kuliko hata walivyotarajia. Kila mtu alimsema yeye,,kila media ilimuongelea yeye KIKI ikawa KIKI kweli
Masaa machache ya kulitangazia taifa kifo chake,,yanageuka mwiba kwake ndani ya sekunde za kuhesabu tu

Mazingira yaleyale yaliyoelezea kifo chake wakati wa kutafuta KIKI,,,kifo kilekile walichotumia kupata KIKI kinageuka jinamizi la kutisha kwao
Mtafutano katika kuiaminisha jamii Ni kweli amefariki na uhalisia wa kuiokoa roho yake kutoka kwa mahasimu ambao walipanga kumuua kweli unazidi kumfanya wema alionje joto la jiwe. Kuishi anataka kifo alichojizushia kinataka kuondoka nae kwa tabasamu.

Ni Vita ya uhai na mauti kwenye ardhi ya viumbe waliokwisha Lia kwenye msiba wake wa kubuni
Ni akina nani wanaotaka kutumia fursa hii ya Kiki kutimiza mauaji yao kwa Wema?

**Jipatie nakala yako kwa shilingi 12000 za kitanzania pekee**
**0742 449 173**
**K I K I**
**Sanaa ya siasa**




**Kitabu: KWA SABABU NAKUPENDA. By Frank Masai**

PENZI lilianzia shuleni; shuleni kabisa, tena Sekondari. Walijikuta wanazama ndani yake na kujiapiza kuwa, "Wakulitenganisha ni MUNGU" tena kwa kifo. Wakajidanganya na kuacha penzi lao lililomea kama magugumaji nyikani lifike machoni mwa walimu. Likawa tatizo.
Daniel Lungwa, anajikuta anaingia matatani baada ya kujihusisha kimapenzi na mtoto wa mmiliki wa shule anayosoma; Josephine Malinzi.
Baba wa Jose anaharibu penzi lao na nusura ayaondoe maisha ya Dan, ni kudra za MUNGU ndizo zinamweka hai yule kijana. Anajiapiza hatoingia penzini tena.
Miaka minne ikatosha kuvunja kiapo chake. Maisha yakamwingiza kwa mara nyingine kwenye mapenzi. Lakini ni afadhali angeingia penzini na mwanamke mwingine, ingekuwa afadhali kubwa. Haikuwa hivyo bwana mdogo akarudisha majeshi kwa yuleyule ambaye ilibaki kidogo ampeleke kwenye nyumba ya milele. Akarudiana na Josephine ambaye kwa muda huo alikuwa msomi wa chuo kikuu huku yeye akiwa dereva bajaji.
Jambo ambalo alilijua wazi, ni kuwa Josephine ana mpenzi mwingine mwenye nguvu kifedha na asiyependa masikhara kwenye mali zake, ikiwemo penzi la Jose. Dan alifahamu fika lakini hakutaka kurudi nyuma. Akala na kusasambua mali za wakubwa. Likawa kosa lingine. Kosa ambalo linagharimu tena maisha yake.
KWA SABABU NAKUPENDA, riwaya inayoangazia suala zima la mapenzi na athari zake katika jamii.
Sasa riwaya hii inapatikana kwa Shilingi 12,000/- za Kitanzania sehemu zifuatazo:-
-Kona ya Riwaya, Kinondoni kwa simu namba 0655428085
-Na popote pale unapotaka kikufikie, piga, tuma ujumbe, whatsapp kwa 0627585638.



05

# KITABU: GAMBA LA NYOKA –Ikisiri (2)

***Kutoka chapisho lililopita, inaendelea...***

**2.0 Mamboleo na Mambosasa**

Hawa ndio wahusika muhimu zaidi katika riwaya hii/ndani ya riwaya. Yaani ndio waliokuzwa zaidi, kuhusishwa na matukio pamoja na maudhui makuu. Tunawashughulikia kwa pamoja kwa sababu wanalingana kwa mambo mengi. Kwanza, wamekuzwa kwa karibu kiwango sawa. Wana kiwango sawa cha elimu, wamekulia na kuelimishwa katika mazingira sawa na wote wawili wanashiriki katika ujenzi wa ujamaa. Hata majina yao ya kimajazi hayatofautiani sana.

Yanadokezea mawazo yao ya kimaendeleo ambayo wanayawakilisha. Mabadiliko yanayohusika ni ya ujenzi wa Tanzania mpya katika misingi ya ujamaa baada ya Azimio la Arusha. Suala hili la kuwamithilisha na mabadiliko ni njia mojawapo ya kufanikisha kuchorwa kwao kitashtiti. Anayechekesha zaidi kati yao ni Mambosasa. Sababu mojawapo ni kwamba anaamini kuwa yeye ndiye kielelezo cha mwanamapinduzi na mzalendo. Lakini matendo yake hayaoani na imani yake. Kwa ujumla, wahusika wote wawili wanajidunisha kutokana na matendo yao.


Baada ya kuhitimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaajiriwa kazi ya ualimu lakini baada ya muda usio mrefu wanapigwa kalamu na kuadhibiwa na serikali kwa kufanya uhalifu mkubwa wa kunajisi na pia kumpiga mwalimu wa siasa wakiwa katika Jeshi la Kujenga Taifa. Ukosefu wa nidhamu na unyama kama huu hauwezi kuhusishwa na uanamapinduzi wala usomi. Kwa kawaida wanamapimduzi ni watu wenye nidhamu ya kiwango cha juu. Aidha, wasomi hutarajiwa kuwa waadilifu. Kutokana na udhaifu wao, Mambosasa na Mamboleo wanajitokeza kama watu duni wasio na uwezo wa kuyafikia yale wanayoyatamani.

Tabia yao ya kiburi ndiyo inayoshambuliwa kitashtiti. Adhabu ambayo Mamboleo na Mambosasa wanapewa na serikali ni agizo la kuishi vijijini kwa muda: "Waishi na watu vijijini ili wapate kuelewa ukweli wa mambo" (uk.61). Kauli hii inadokeza kwamba ijapokuwa wao ni wasomi, hawajui uhalisi wa maisha.

Wakiwa kijijini, udhaifu wao unazidi kudhihirika kutokana na kushiriki kwao katika mambo ambayo ni ya kuchekesha na kuchukiza wakati mwingine. Kwanza, wanavunja matumaini ya wanakijiji. Hii ni kwa sababu katika kijiji cha Bucho, wao tu ndio wenye elimu ya chuo kikuu. Kwa sababu hii, wanakijiji wanawathamini sana na kujawa na matumaini kwamba wataenda mbali maishani na wataleta ustawi utakaowanufaisha wote. Hivyo, wanakijiji wanawachagua kuwa viongozi wao. Mambosasa anachaguliwa kuwa mwenyekiti, na Mamboleo kuwa katibu.

Lakini wanashindwa kuzitumia nyadhifa hizi kuleta mabadiliko ya kuwanufaisha wanakijiji. Mambosasa anatumia wadhifa wake kupora pesa za kijiji. Mamboleo anapomlaumu, anajitetea kwa njia ya kuchekesha. Anadai kuwa amekatishwa tamaa na viongozi wa juu serikalini, ambao ni mafisadi. "Inabidi nami nianze kuwa kama wao," anasema (uk. 85). Hiki ni kisingizio cha kufichia uovu wake wa kushiriki katika ufisadi. Ni wazi kwamba uzandiki wake ndio unaopigwa vita hapa. Hatimaye, Mamboleo na Mambosasa wanaondolewa katika uongozi wa kijiji kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo.

## PITIO LA VITABU




Viongozi wapya wanachaguliwa, na ndio wanaoleta ustawi kijijini. Chini ya usimamizi bora wa Kamala, kijiji cha ujamaa cha Bucho kinaishia kuwa kijiji bora zaidi wilayani (uk.112). Uongozi wa wasomi unagotanishwa na ule wa mwanakijiji wa kawaida, yaani Kamala, ili kuubeza na kutilia mkazo ulivyoshindwa.

Tukio mojawapo la kuchekesha zaidi ambapo Mamboleo na Mambosasa wanahusika ni makabiliano kati yao na Padri Madevu. Wanakwenda nyumbani kwake kumkemea kwa sababu ya mahubiri yake ambayo yanawapotosha wananchi.

**Ikisiri hii imechukuliwa mtandaoni na imeandikwa na Mwenda Mbatiah**

# -SAIKOLOJIA-
# PAMBANA NA MAUMIVU YA MOYO

**Neema Mgao**

**Simu+255763013206.**
**What's app no.**
**+255746139654.**
**DODOMA**
**TANZANIA.**



**PAMBANA NA MAUMIVU YA MOYO. YAPOKEE,JITIBIE MAUMIVU HAYO.**

Ngoja nikuulize, umeshawahi kuumia moyoni?
Umeshawahi kuumizwa moyo?
Umeshawahi kuumiza moyo wa mtu?
Maumivu ya moyo ni nini?

Kwanza tujue maumivu ya moyo ni nini, tunasikia watu wakisema moyo unauma, sasa tujue moyo kuuma ni kitu gani.
Maumivu ya moyo ni ile hali ya kujihisi kuumia saana ndani ya moyo wako iwe ni kwa kujipa hatia au kwa kujipa onyo. Au kwa kujihukumu. Au, Maumivu ya moyo ni ile hali ya moyo kuhangaika na kutokutulia kutokana na kufanyiwa jambo fulani hasa hasa liwe la kuumizwa moyoni hadi fikrani.

**Nini husababisha maumivu ya moyo?**

Kama tulivyoona kwenye maana kuwa maumivu ya moyo husababishwa, basi tuone baadhi ya sababu zitakazosababisha mtu kupata maumivu hayo

a). Kusalitiwa
Hii sana sana huwa katika mapenzi ndio unaweza kuisikia vizuri, yule mpenzi uliyempenda sana ukashuhudia usaliti kutoka kwake moyo huuma.

b). Kudhurumiwa.
Ile hali ya kudhurumiwa ama mali yako, heshima yako, au utu wako pengine kwa kudhurumiwa na wale uliowatendea mema, nayo ni hali inayoweza kusababisha maumivu ya moyo.

c). Kukumbuka mabaya uliyoshindwa kuyasamehe.

Hii nayo inaweza kuwa sababu ya moja kwa moja ya kukusababishia kupata maumivu ya moyoni. Ile hali ya kuhifadhi maumivu bila kusamehe na kuyaachilia inaweza kukusababishia kupata maumivu ya moyo kila utakapokumbuka jambo lililokuumiza.

Hizo ni baadhi tuu ya sababu zinazoweza kukusababishia maumivu ya moyo.

Pambana na maumivu ya moyo utakayokumbana nayo, wakati mwingine unaweza kukutana au kupambana na maumivu ya moyo kwa kiwango kikubwa saana. Yahimili hayo maumivu, usiruhusu yakakuendesha hata kukupelekea kufanya mambo yatakayotafsiriwa kuwa ya ajabu. Dhibiti maumivu unayoyasikia moyoni, iwe yametokana na sababu yoyote, iwe hizo nilizoziainisha au nyinginezo jitahidi kuzidhibiti ili zisikuathiri na kukupa maumivu ya moyo wako.

Pambana na hayo maumivu ndani ya moyo wako, himili hayo maumivu ili yasikuletee athari ndani ya moyo wako.

**YAPOKEE HAYO MAUMIVU.**
Pokea hayo yanayosababisha maumivu ndani ya moyo wako. Ikiwa ni maumivu yatokanayo na usaliti, sema na moyo wako, iambie nafsi yako kuwa huyo aliyekusaliti haikua riziki yako kuwa nae, jisemeshe wewe mwenyewe ili usiiumize nafsi yako juu ya usaliti. Pokea maumivu hayo, japo ni ngumu ila pokea kuumia, pokea kupondeka, pokea kuumizwa ili nafsi yako isiumie sana.

Pokea kuumizwa, ili moyo wako uwe salama. Unajua kuna watu pengine hata hao wa karibu yako, lazima watakuumiza. Amini kwamba kuna watu wanachukia wewe ukicheka, yaani kukuona wewe una furaha hawataki kabisa. Furaha yao ni uwe unanung'unika kila wakati. Yaani pengine hata ndugu yako wa damu, inamsumbua sana anapoona unafurahi, ila ukiwa unaumia yeye ndio anafurahi, na mbaya zaidi, utakapoonesha kuumia basi pengine akawa karibu na wewe lakini kwa lengo la kuwa ahakikishe unaumia sawasawa.

# -SAIKOLOJIA-
# PAMBANA NA MAUMIVU YA MOYO

Pokea maumivu. Mshangaze anaetegemea kuwa kwa kuwa umeumia utakaa chini na kulia, mshangaze kwa kuyapokea maumivu.

**JITIBIE MAUMIVU HAYO.**
Wakati mwingine, kuna maumivu tunashindwa kuyazuia yasitupate. Tunajikuta tumepokea kuumia, tunajikuta tumeumia haswaa, yaani wakati mwingine tunaumia hadi tunaumwa na mwili na kun-yong'onyeshwa nafsi. Ukishayapokea maumivu, hatua ina-yofwata ni kujitibia hayo maumivu. Tuone baadhi ya mambo am-bayo tunaweza kufanya ili kujitibia hayo maumivu ya moyo.



1. Zungumza na moyo wako.
Ni sawa umeumia, ndio umeumizwa. Ni kweli mi sijui ni namna gani unaumia, ni kweli inau-ma, nikwambie tu, zungumza na moyo wako, zungumza na akili yako. Kuna mawasiliano ya moja kwa moja kati ya moyo wako na akili yako. Akili ni sawa na DVD, halafu moyo ni sawa deki, sasa ili DVD isome ni wazi kuwa inatakiwa iwekwe kwenye deki.

Hivyo moyo na akili hutegemeana, sasa jitahidi kuzidhibiti hisia na fikra zako ili kuuepusha moyo zungumza na moyo wako ili kuupooza pale una-popata maumivu.

2. Tafuta njia za kujifariji.
Moyo unapopata maumivu makali, jitahidi kutafuta namna ya kuufariji. Unaweza kuufariji kwa maneno mf. Kama ni maumivu ya moyo yanayotokana na mapenzi, unaweza jiambia *"bwaana eehh, mwanaume au mwanamke hayupo peke yake"*, kauli hizo huashiria kupuuzia. Nakuhakikishia ni nafuu ya mpuuziaji kuli-ko yule ambae kila jambo ye anahifadhi moyoni,kitu kidogo tuu kahifadhi. Puuzia.

Mtu anaposhindwa kupambana na maumivu ya moyo anaweza kupata madhara mbalimbali, lakini haya ni baadhi.

*Kupata msongo wa mawazo.
*Kukosa amani.
*Kuwa na hasira muda wote.
*Kuwa mkali mkali muda wote.
*Kukosa upendo.
Madhara hayo na mengineyo yanaweza kujitokeza pindi mtu anaposhindwa kupambana na maumivu ya moyo wake.

TUJITAHIDI KUPAMBANA NA MAUMIVU YA MOYO.TUOMBE MUNGU ATUONGOZE KATIKA KUPAMBANA NA MAUMIVU YA MOYO. ASANTE.




# HADITHI: NILIMUUA DADA NIOLEWE NA SHEMEJI-08



Na. Makoleko Kalibonge

*Ilipoishia*

**Niliona kama mpango unaelekea kushindikana. Sikuona kama kumpata kunguru aliye hai itakuwa rahisi. Nikiwa katika mawazo hayo, nilipitiwa na usingizi. Sikufahamu kama nilikuwa naota ama la.**

***Tuendelee***

Ninachokikumbuka ni kuwa, nikiwa katikati ya usingizi niliota niko barabarani namuwinda kunguru ambaye alikuwa ametua juu ya nguzo ya umeme. Nilimnyatia nikamkaribia. Nilipotaka kumkamata aliruka huku akilia "Koo! Koo! Koo!" Aliporuka huku akilia hivyo nilichukia sana. Wakati nikiwa bado usingizini nilisikia mlio wa kunguru niliyemkosa. Nilishtuka usingizini. Ajabu niliendelea kuisikia ile sauti. Nilijifunua shuka kuisikiliza kwa makini. Bado iliendelea kusikika tena ilikuwa inasikika upande wa dirishani kule chumbani. Nilitoka kitandani kuanza kutembea taratibu kuelekea upande wa dirisha hadi nikalifikia. Hapo niliisikia kwa karibu sana. Nilifungua dirisha kuangaza nje, nikamuona kunguru ametua katika kona moja ya dirisha. Ajabu ni kwamba hakukimbia wala kuniogopa. Aliendelea kutulia.

Nilinyoosha mkono nikamdaka bila shida. Alikuwa mtulivu ajabu. Wakati namtia mikononi aliacha kulia. Nilistaajabu sana. Nilimtia kwenye mkoba nilioweka nguo ya ndani ya dada. Kisha nilirudi kitandani kulala.

*** * ***

Siku iliyofuata niliamka mapema sana. Nilifanya kazi zangu kama kawaida. Moyoni nilikuwa na matumaini makubwa juu ya mpango wangu. Nilipohakikisha nimemaliza kila kitu, niliingia bafuni kuoga. Nilipotoka bafuni nikajiandaa vizuri, halafu nikawasubiria watu wengine waamke. Mtu wa kwanza kuamka alikuwa baba, akafuatia mama kisha dada. Walipoona mazingira ya ndani yako safi kiasi kile walishangaa sana. Mi' sikuwa na habari nao. Niliendelea na maandalizi yangu. Nilipomaliza kujiandaa, nilichukua mkoba wangu ambao ndani mlikuwa na kunguru na nguo ya ndani ya dada. Niliupachika begani nikatoka zangu hadi Mwenge ambako nilipanda daladala hadi Bagamoyo.

Nilipofika nilimkuta mtaalamu wangu akiwashughulikia watu wengine. Nilikaa kwenye foleni kusubiri zamu yangu. Zamu yangu ilipofika niliingia ndani. Yule mganga aliponiona alianza kucheka. Kicheko chake hadi leo nakusimulia mkasa huu sijafahamu alikuwa anacheka nini.

"Karibu!" Alinikaribisha kama alivyofanya jana akinielekeza namna ya kukaa. Nilikaa kama alivyonielekeza huku tukielekeana. Nilipokwishakaa aliniuliza, "Vipi mahitaji yangu umekamilisha?"

"Ndiyo babu. Haya hapa." Nilimjibu huku nikinyoosha mkono kumkabidhi ule mkoba. Aliupokea na kuangalia vilivyomo.

"Safi sana," alisema. Alimtoa kunguru ambaye tangu nimemuweka usiku wa jana hadi sasa hajatoa sauti. Baada ya kumtoa alimuweka pembeni yake. Aliingiza mkono mkobani tena akaitoa nguo ya ndani akaiweka karibu na kunguru. Alipomaliza kufanya hivyo alitoka nje ambako baada ya dakika chache alirejea akiwa na beseni la maji, akaliweka mbele yake. Alichukua kichupa kidogo. Alikifungua akamimina kitu mfano wa poda. Aliijaza katika mfuniko wa kichupa kisha aliimiminia kwenye beseni la maji. Alichukua kichupa kingine akafanya vilevile na kutia kwenye maji.

Alipokwishafanya hivyo alichukua mkoba wake wa ngozi. Aliufungua akaingiza mkono. Humo alitoa vitu mithili ya vipande vya mti. Alikichukua kipande kimoja akakivunja katikati kisha alivitosa kwenye beseni. Baada ya muda mfupi yale maji yalibadilika rangi. Yalikuwa kama rangi nyekundu. Alimchukua kunguru akamchinja. Damu akainyunyizia kwenye nguo ya ndani ya dada kisha nguo hiyo aliitosa kwenye maji. Baada ya kuitosa akawa kama anaifua.

Kadiri alivyokuwa anafikicha ile nguo, maji nayo yalibadilika rangi na kuwa kama hapo awali. Aliacha kuifikicha ile nguo, akaikamua na kuiweka pembeni. Akaniambia nisogee karibu na beseni. Nilipolisogelea akachukua usinga akautosa kwenye

maji na kuyakoroga. Alifanya hivyo huku akisema maneno ambayo sikuyaelewa. Alipomaliza kufanya hivyo aliyaacha yatulie. Kadiri yalivyokuwa yanatuama maji yale niliona kama picha ya mtu ambayo ilikuwa inaunganika kila maji yalipokuwa yanatulia. Baada ya muda nilipata picha kamili. Jamani duniani kuna mambo. Picha niliyokuwa naiona ilikuwa ya dada yangu ambaye nimemuacha nyumbani. Ilionekana vizuri sana akiwa na ujauzito wake. Maji yalipotulia kabisa mganga aliniambia ninuwie juu ya nikitakacho huku nikiingalia ile picha. Shetani alipepea kila mara.

Sikuwa na huruma, nililiinamia beseni la maji ambayo yalionesha picha ya dada. Nikanuia. Nilipomaliza kufanya hivyo, mganga alinipa kisu akaniambia niyakate maji kwa namna ya kuweka mkasi. Nikishafanya hivyo nimalize kwa kuchoma katikati ya maji. Nilikipokea kisu nikafanya kama nilivyoagizwa. Nilianza kuweka mkasi halafu nikajiandaa kuyachoma yale maji katikati. Niliunyanyua mkono juu. Kabla sijaurudisha ghafla nilimuona dada akinyoosha mikono yake kama mtu aombaye msamaha. Kwa namna alivyonyoosha mikono ilionesha alikuwa katika maumivu makali. Alilalamika sana. Moyo ulilipuka puuh. Ujasiri ulipotea hata kisu kikaniponyoka na kuangukia chini. Niliingiwa na huruma. Nilimwambia mganga siwezi kuendelea na zoezi lile. Nilimtaka afanye utaratibu mwingine. Mawazo yangu yalishabadilika baada ya kumuona dada katika hali ile. Nilitamani kusitisha mpango ule.

Mganga aliniambia kuwa lazima niimalize kazi niliyoianza. Alisisitiza halitositishwa kwa sababu ya vile nilivyofanya mara ya kwanza. Haikuwa kazi rahisi kuiacha. Kama nitafanya hivyo, nijiandae kufa mimi na dada atabaki kuwa zezeta kutokana na kumjeruhi sana. Pia kama sitokufa itafika wakati dada atasimulia kisa chote. Kufikia hapo sikuwa na chaguo tena zaidi ya kumalizia. Nilikiokota kisu nikakipeleka juu halafu nilikirudisha kwa kasi ya ajabu kuyachoma yale maji. Nilimsikia dada akilalamika, "Mdogo wangu unaniua." Palepale niliyaona maji yakibadilika rangi na kuwa damu tupu. Niliiona taswira ya dada ikitapatapa halafu ikapotea taratibu. Hatimaye ilitoweka kabisa.

Zoezi hilo lilipokamilika, mganga aliuchukua mkoba wake akaingiza mkono ndani yake akatoa kichupa kidogo ambacho hakikuwa na kitu ndani yake. Alikiweka karibu na beseni. Aliuweka mkoba mahala pake kisha alisimama. Alichukua baseni akamimina yale maji yaliyobadilika kuwa damu kutia kwenye kile kichupa.
Hapo nilishuhudia maajabu mengine. Maji au niseme damu iliyokuwa kwenye beseni iliingia yote kwenye kichupa. Halikubaki hata tone. Alipohakikisha yameingia alikifunga kisha alinikabidhi. Aliniambia nizunguke nyuma ya kile kibanda nitaukuta moto nikitose kile kichupa halafu nirudi ndani bila kugeuka nyuma. Nilikipokea nikafanya kama nilivyoagizwa halafu nikarudi ndani.

Nilipokuwa nakaa tena katika mkao wangu baada ya kutoka nje, nilisikia mlipuko mkubwa sana kutoka nyuma ya kibanda. Mganga aliniambia kuwa kazi imekwisha. Kilichobaki ni kumtengeneza shemeji kutumia kunguru. Nikaruhusiwa kuondoka lakini kwa sharti la kutogeuka nyuma hadi nitakapofika nyumbani. Niliagana naye mikashika njia yangu hadi kituo cha daladala ambako nilipanda gari kurudi nyumbani.

*** * ***

Nilikuwa makini sana katika kutekeleza maagizo ya mganga. Nilipotoka kwake, sikugeuka nyuma mpaka nikafika kituo cha daladala. Nilipanda kwenye daladala na kukaa kimya nikitafakari mambo niliyokutana nayo. Nilimuona dada vile alivyokuwa akitapatapa kwenye beseni la maji kwa mganga. Niliiona damu yake ilivyobadilisha rangi ya maji hata vile alivyokuwa anatoweka taratibu kwenye yale maji huku akipiga kelele za maumivu makali yaliyokuwa yanamkabili.

Niliyakumbuka mambo yake mema aliyonifanyia wakati niko mdogo, nilipokuwa shuleni hata alipoolewa hakunitupa. Katu sikuliona kosa lake hata marejesho yake yawe haya niliyomrejeshea. Roho iliniuma sana. Nilijishangaa kwa nini nilikuwa mtu mbaya niliyetekeleza kila nililolipanga tena kwa haraka na wepesi namna hii.
Nilikuwa mwepesi wa kusahau fadhila na mwepesi wa kulipa madhila. Nilimpenda sana dada yangu. Sijui ni shetani gani aliniganda katika moyo wangu hata nikajikuta nakuwa mtumwa wake kwa kiasi kikubwa. Sikukumbuka Mwenge tulifika wakati gani. Nilichokikumbuka ni kudaiwa nauli na konda.
***Itaendelea!***

# MIAMBA WA AFRIKA

## Samora Machel - 07

Wakati waliouawa walikuwa wanachama wa mlengo wa kijeshi wa ANC, Umkhonto we Sizwe (MK - Spear of the Nation), nyumba hizo hazikuwa kambi ya waasi, kama wanadiplomasia na waandishi wa habari waliozuru walithibitisha hivi karibuni. Wiki moja baadaye, Machel alitupa goli. Katika mkutano wa hadhara katika uwanja wa uhuru wa Maputo, alimkumbatia kiongozi wa ANC Oliver Tambo na kutangaza "Wanataka kuja hapa na kufanya mauaji. Kwa hiyo tunasema: Waache waje! Waje!... Waje Waafrika Kusini, lakini wajue wazi kwamba vita vitaisha Pretoria!"

Ikisaidiwa na silaha zilizorushwa na Jeshi la Ulinzi la Afrika Kusini (SADF), Renamo ilieneza oparesheni zake kote nchini isipokuwa eneo la kaskazini la mbali. Frelimo ilijibu kwa msururu wa hatua za kimabavu, ambazo baadhi yake ziliwashtua sana wafuasi wake ndani na nje ya nchi. Adhabu ya kifo, ambayo tayari inatumika kwa makosa makubwa ya usalama, sasa iliongezwa hadi kwa uhalifu wa kiuchumi. Aidha, adhabu ya viboko ilitolewa kama adhabu kwa makosa mbalimbali. Sheria zote mbili ziliacha kutumika ndani ya mwaka mmoja au zaidi lakini zilifanya uharibifu mkubwa kwenye sura ya Frelimo. Inaaminika kwamba, karibu wakati huo, maafisa wa zamani wa Frelimo waliochukuliwa kuwa "wasaliti" waliuawa, akiwemo Simango na mkewe Celina. Hadi leo, Frelimo haijachapisha chochote kuhusu mazingira ya kunyongwa, ingawa katika bunge la Msumbiji, mwaka 1995, waziri wa zamani wa usalama Sergio Vieira alithibitisha hadharani "wasaliti waliuawa". Wafuasi wa RENAMO walichapisha matoleo ya rangi wakidai kuwa mauaji yalifanyika mwaka wa 1977, lakini mwaka 1983 unaonekana kuwa na uwezekano zaidi. Kwa vyovyote vile, hii ilikiuka ahadi ambayo Machel aliwapa Marais wa Tanzania na Zambia, Julius Nyerere na Kenneth Kaunda mwaka 1975.



Katika Kongamano la Nne la FRELIMO, mnamo Aprili 1983, chama hicho kilithibitisha kujitolea kwake kwenye harakati za Umaksi, lakini ilikubali makosa ya kiuchumi, hasa katika kilimo. Machel alichaguliwa tena kuwa Rais wa chama hicho, na kwa mara nyingine tena akamkumbatia Oliver Tambo.

Lakini kuzorota kwa hali ya kijeshi na kiuchumi kuliisukuma Frelimo kuipa serikali ya ubaguzi wa rangi kile ilichosema ilitaka - mkataba wa kutotumia nguvu. Mnamo Machi 16, 1984, kwenye gari la reli katika ardhi isiyo ya watu kati ya Afrika Kusini na Msumbiji, Machel na Rais wa Afrika Kusini P. W. Botha walitia saini Mkataba wa Nkomati wa Kutokufanya Uchokozi na Ujirani Mwema. Mkataba uliooneshwa katika makubaliano hayo ulikuwa rahisi sana - Afrika Kusini ingeacha kuunga mkono Renamo badala ya Msumbiji kuacha kuungwa mkono na ANC.
Machel alitimiza kwa kiasi ahadi za kuwafukuza wanachama mbalimbali wa ANC kutoka katika eneo lake. Msaada wa Afrika Kusini kwa Renamo haukukoma - shehena kubwa za silaha zilisafirishwa kwa ndege hadi Renamo mara moja kabla ya Mkataba huo, na afisa mkuu wa Afrika Kusini, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje Louis Nel, alitembelea kituo cha Renamo huko Casa Banana wilayani Gorongosa, kwa kutumia uwanja wa ndege ambao Afrika Kusini ilisaidia kujenga Renamo. Katikati ya 1985, wanajeshi wa Msumbiji na Zimbabwe walianzisha mashambulizi ya pamoja ili kuwafukuza Renamo kutoka Gorongosa. Askari wa miamvuli wa Zimbabwe walihakikisha kukamatwa kwa Casa Banana, lakini kiongozi wa Renamo Afonso Dhlakama alikimbia kaskazini, na kuanzisha tena Makao Makuu ya Renamo katika wilaya ya Maringue.

***Itaendelea...***

# SAKO KWA BAKO: ANNA MELEIYA MBISE—02

## Msomaji, Mhamasishaji, Mwandishi wa Riwaya na Mshairi

**Leo tunaendelea na mazungumzo yetu na Bi. Anna Meleiya Mbise. Maswali kadhaa ya papo kwa papo yatakufanya umjue zaidi… huyu hapa na leo anajibu swali la 5 na 6 kati ya 10 niliyomuuliza.**

**5. Kwako wewe kitabu ni nini?**

Kitabu ni moja ya zana za ukombozi wa kifikra, kiutamaduni, kiuchumi na kisiasa. Pamoja na kuwa huwa natumia njia nyinginezo kujipatia taarifa na maarifa, vitabu vimekuwa na mchango mkubwa sana kwenye maisha yangu hasa katika kunisaidia kufanya maamuzi katika mambo mbalimbali, kutoa ushauri na kuelimisha wengine pale inapohitajika na vilevile kunipa burudani.

Kuna wakati unasoma kitabu unakuwa unacheka mwenyewe kama mwehu, kutokana na mpangilio na mfululizo wa matukio, yaani unakuta kitabu kimekushika unahisi ukikiweka chini utaugua basi unaendelea kukisoma mpaka unakimaliza uweze kupata uhondo wote ukiwa wa moto, raha ya vitabu bwana!



**6. Zaidi ya vitabu nini kingine unapenda kufanya?**

Mimi ni rafiki wa mazingira, napenda sana bustani za mbogamboga, maua na ufugaji. Nina bustani za maua, mboga mboga na ufugaji. Yaani asubuhi nikiamka baada ya kusalimia watu wa nyumbani kwangu lazima nitoke nje nisalimie mimea na mifugo.

Napata raha sana, nikiangalia maua, mboga na mifugo yangu naona kama vinanitegemea na hivyo nahitaji kujua changamoto zilizopo nizitatue. Vilevile, mimi ni mpenzi wa kusafiri, napenda kusafiri ndani na nje ya Tanzania. Ninaposafiri hata ndani ya Tanzania huchunguza sehemu muhimu kwenye mkoa ninaoenda na kupanga kuzitembelea, sawa sawa na nnavyosafiri nje ya nchi. Sehemu muhimu sana ambazo nikisafiri lazima nizitembelee ni sokoni.

Haya masoko ya wazi ya wakulima na vie vile maduka ya vitabu na makumbusho. Nikitembelea sehemu hizo huwa naweza kupata picha kubwa ya jamii husika na kuweza kuongea na watu mbalimbali, napenda kupiga soga sana.

**7. Je umeshawahi kufikiria kuandika kitabu!? (Kama ndiyo... Ni cha utanzu upi!)**

Ndio, nimeshaandika na kuchapisha mashairi mbalimbali kama vile shairi la “Udugu wetu matatani”, “Kiswahili Lugha Tamu” “Love me Now” na “Abnormal”. Niko mbioni kumalizia Diwani yangu “Mbiu – UTU Taabani” ni kitabu cha ushairi chenye mashairi ya Kiswahili zaidi ya 50. Wasomaji kaeni chonjo kikitoka muweze kukisoma. Nina kitabu cha Watoto pia ambacho kitatoka mda si mrefu, cha lugha ya Kiswahili na Kingereza kiitwacho “Sisi Watoto Tunajali UTU” wazazi jiandaeni kukisoma pamoja na watoto wenu. Naandika pia kitabu cha self-help kiitwacho “Life that Matters” vyote vinatarajiwa kumalizika ndani ya mwaka huu. Kadhalika, nimeshaandika Makala na machapisho mbalimbali kuhusu elimu na teknolojia, hifadhi ya jamii, na masuala ya jinsia na haki kodi.

*Makala hii itaendelea toleo lijalo*

Anna Meleiya Mbise (Facebook, Twitter, Linkeln na Tiktok)
Email:annambise2015@gmail.com
+255766069962

**Jiunge na Anna Mbise Mobile Library, ujisomee vitabu kwa soft copy au Hard Copy wakati wowote popote ulipo Tanzania. Wasiliane naye kwa simu namba hiyo hapo juu uhudumiwe.**

# MPIGAMBIO — 23

*Ilipoishia...*
**"Mpo nyumbani kwangu, nikiamua hapa haondoki mtu hata kama mtamwita OCD… nimesema ninamleta kwa kuwa tu ninawaheshimu… nyi nendeni mi nakuja naye!" akawaambia, "Prisca, toa viumbe wako hapa!" akamwambia Prisca aliyekuwa kajiinamia muda wote.**

*Endelea...*
Wale askari wakabaki kimya wakitazamana kiwiziwizi, hawakujua Kenny anajiamini nini kwa maneno yake.
"Utamleta kweli?" yule WP akauliza.
"Nendeni mkatusubiri! Namleta muda si mrefu, halafu mbivu na mbichi zitajulikana hukohuko!" akawaambia.
Wale askari wakaaga na kuondoka na Prisca. Kenny akatulia kwa sekunde kadhaa baada ya wale askari kuondoka.

"Hivi huyu mwanamke anakutakia nini?" Kenny akamuuliza Ikunda.
"Nahisi anaitaka roho yangu!" Ikunda akajibu akiwa tayari sebuleni.
"Mi niko tayari, ila naogopa Kenny,"
"Usiogope, twende na hawatakufanya lolote!" Kenny akamtoa hofu mpenziwe. Wakatoka na kuingia kwenye Crown lililokuwa nje limeegeshwa.

*** ***

"Vipi! Mmefanikiwa?" sauti ya Habibu kwenye simu ilimuuliza Prisca.
"Wamesema wanakuja wenyewe kituoni"
"Ye na nani?"
"Na mpenziwe Kenneth!" Prisca akajibu. Upande wa pili Habibu akasonya, "Sipo mbali, nimeegesha gari mtaa wa pili, nataka niwaone halafu niamue la kufanya…" Habibu akajibu na kukata simu. Kisha akaondoa gari lake kutoka pale alipoliegesha na kulisogeza upande wa pili kulikokuwa na kituo cha polisi.

Prisca aliliona gari la Kenneth likiiacha barabara kuu na kuingia kwenye maegesho ya kituo hicho. Akainuka kutoka pale alipoketi, kana kwamba anataka kuwapokea watu hao.
Kenny na Ikunda waliteremka wakashikana mikono kuelekea dawati la mapokezi la kituo hicho.
"Karibuni!" askari aliyekuwa hapo akawakaribisha na wakati huohuo Prisca aliingia pale mapokezi.
"Anhaa ndiyo watu wako ee?" yule afande akamuuliza Prisca aliyejibu kwa kichwa. "Haya ingieni mlango huo…"
"Haina sababu, huyo mwanamke awekwe ndani kwanza…" sauti kutoka kwenye like chumba ilisikika. Ikunda alihisi haja zote zinataka zitoke. Kenny hakuonekana hata kutetereka. Akamshika mkono Ikunda na kuingia naye ndani ya kile chumba.
"Mliyemfuata nimemleta huyu hapa!" Kenny akamwambia yule askari aliyekuja nyumbani kwake, Mara hii akiwa ofisini kwake.
"Sawa tunashukuru, lakini inabidi awekwe ndani na kesho apandishwe mahakamani!" yule askari akaongea huku akiandika kwenye jalada fulani.
"Kwa hiyo mtu huwa anawekwa ndani bila kuchukuliwa maelezo na kuambiwa kosa lake?" Kenny akauliza.

"Usinifundishe kazi!"
"Sikufundishi nakukumbusha tu yale uliyofundishwa CCP Moshi…"
"Nikiamua na we ntakuweka



Richard Mwambe

ndani…"
"Unasema?" Kenny akauliza, "hebu niangalie vizuri…" yule kijana akainua uso kumtazama. "Fanya kazi kwa weledi… kazi ya jeshi la polisi ni kulinda raia na mali zao, na si kuwakandamiza, kuwabambikia kesi na kuwaweka ndani bila mashauri. Kila siku serikali inalalamika mahabusu zimejaa lakini yote ni kwa uzembe wenu," Kenny akazungumza kwa maneno makali yaliyomfanya yule askari kuhamaki na kujiuliza nani anayeongea naye. Kenny akachukua simu yake na kubofya namba fulani, akaiweka sikioni.

"Shikamoo mzee!" akasalimia.
"Marhaba kijana hujambo?" sauti ya upande wa pili ikaitika kizembe.
"Nipo hapa kituo cha polisi Mikocheni…"
"Kuna nini tena kijana, we hutakiwi kuonekana maeneo hayo ni hatai kwa afya yako…" mtu wa upande wa pili akajibu kwa kukatisha sentensi ya Kenny.
"Ndiyo, kuna shauri la mchumba wangu hapa nimekuja kulishughulikia… lakini vijana wako wananionea sana, hawataki kuchukua maelezo wala nini, wanang'ang'ania kumweka ndani…"

# MPIGAMBIO — 23



"Nyoka! Subiri kidogo…" ile simu ikakatwa. Yule askari pale kitini akashikwa na degedege la dharula.
"Mambo gani sasa hayo?" akaanza kumlalamikia Kenny.
"Nyi si hamtaki kufanya kazi kwa weledi, wacha tuwaambie walimu wenu wawafundie tena" Kenny akawaambia.

Haikupita hata dakika mbili, Mkuu wa kituo hicho akafika kaunta, "yuko wapi huyo nyoka?" akauliza. Wale askari wakashangaa hilo jina. Kenny alisikia kutoka huko, akajitokeza "Mimi huku mzee!". Yule Mkuu wa kituo akaingia ndani ya ile ofisi na radio kolu yake mkononi. Yule kijana akasimama na kupiga saluti, akawa mdogo kama punje ya haladali.
"Shida nini mpaka wakubwa wanapiga simu? Hivi hamjui mtatuletea matatizo humu ndani, enh!" akakoroma yule Mkuu.
"Ha-ha-pana mkuu… tttunashughhulikia…" akajibu kwa woga.

*Kumbe wakiwa wakubwa zenu mnalowa!* Kenny akawaza. Yule Mkuu akamgeukia Kenneth. Macho yao yakagongana.
"WEWE!" akamwambia Kenneth. Kijana yule akamtazama yule mzee, naam, sura zilikutana mahali.
"WEWE!" akarudia tena. Kenny akatulia tuli akimtazama yule askari kwenye cheo kikubwa pale kituoni.
"Ndiyo, mimi!" Kenny akajibu.
Yule Mkuu akamgeukia yule askari wake. "Chukua maelezo ya huyo mchumba 'ake na huyo anayemshitaki, kisha niletee wao wote wawili, na hayo maelezo na wewe mwenyewe na huyo WP aliyeshika kesi, niwaone ofisini, nawapa dakika kumi tu…" akamgeukia Kenny.
"Unanikumbuka?" akamuuliza.
"Siwezi kukusahau, *never*!" Kenny akajibu.
"Twende ofisini…"

Kenny na yule OCD waliongozana mpaka ofini. Walipoingia ndani wote wawili akaufunga mlango kwa ufunguo. Kenny alisimama upande wa pili huku yule Mkuu wa kituo upande mwingine.
Bila simile, yule Mkuu wa kituo akmkwida shati Kenny na kumtikisa huku kaubana mdomo wake wa chini kwa meno yake.
"Mshenzi sana wewe! Ulifikiri utanikimbia? Ndani ya dunia hii ulifikiri utanikimbia?" yule askari akafoka mishipa ikiwa imemdinda usoni. "Na aliyekutoa jela hakufikiri kabisa kama wewe ni kiumbe hatari, kwanini hakukuua hukohuko? Son *of bitch!*" akaendelea kufoka. Kenny alitulia kikwido kile kikiwa kinaendelea. Si kwamba hakuweza kupambana naye lakini kuna lililomfanya abaki kuwa mpole. Alipoachiwa aliliweka sawa Shari lake na kujikohoza kidogo. Akiwa hajakaa sawa, alishtuka akipigwa ngumi moja nzito iliyotua sawia shavuni. Kenneth aliyumba kiodogo na kusimama imara.

"Benson! Hivi unajua ni kosa la kisheria kumpiga au kupigana na mtu mbele ya picha ya Rais?" Kenny akamwambia.
"Usinifundishe mpumbavu wewe! Na nitakuua, nyamafu!" akalalama kwa hasira.

*** *** ***

Benson Msusa, Mkuu wa kituo cha polisi cha Mikocheni alifahamiana na Kenneth miaka zaidi ya kumi na tano nyuma kwenye tukio baya kabisa la ujambazi lililotokea ndani ya hoteli moja huko Mererani.
Na tukio hilo ndilo lilikuwa la mwisho kuwakutanisha wawili hao.
Benson na Kenneth walikuwa marafiki sana katika biashara zao halifu. Asubuhi ya siku moja wawili hao walikuwa wakimvizia tajiri mmoja wa Kihindi aliyekuwa na mzigo wa Tanzanite wenye thamani ya shilingi za Kitanzania Milioni mia moja.

Katika baa ya Maganzo Benson alikaa meza moja na Kenneth, "umepangaje?" Benson alimuuliza Kenny.
"Kuna malaya nimemsukumia, akiingia naye geto tu, tunaenda…" Kenny akajibu.
"Mzigo anao hotelini?"
"Biashara inafanyika leoleo… kuna jamaa wanakuja kununua mzigo so na sisi tunapiga hapohapo…" Kenny akaeleza.
Mazungumzo yakaendelea.
Dakika ishirini zilizofuata Kenny akapewa ujumbe kuwa biashara imeshafanyika.
"Twende!" Kenny akamwambia Benson. Kila mtu akahakikisha bastola yake ipo sawa.
Wakainuka na kuingia garini safari ikaanza.

**Chapisho lijalo litakuwa la mwisho hapa jaridani. Baada ya hapo kitabu kitapatikana.**

**Ilipoishia…**

**Mwendo wa kama dakika ishirini hivi, aliegesha gari pembeni, akachukua simu yake na kuiwasha, akaenda kwenye GPS Locator na kuangalia kama yuko kwenye njia sahihi au kakosea. Yuko sawa na tayari alikuwa amefika eneo hasa analolitaka.**

***Endelea...***

Akiwa anaendesha gari lile taratibu akakutana na mtu mmoja aliyekuwa akivuta mkokoteni akielekea upande ule ambao yeye anatokea.

"Helo, samahani bwana, eti nyumba ya Zuganji Kumeil unaijua?" akauliza. Yule bwana badala ya kumjibu akamkodolea macho kama haelewi alichoambiwa. Na fahamu zilipomrudia akatabasamu.

"Unataka kwenda kwa huyo 'Nyonya Damu?'" akauliza.

"Nyonya damu?" Colbas akauliza.

"Ndiyo, we binadamu gani asiyetaka ushirikiano na wenzake? Ongoza tu baada ya villa utafika kwa junction, fuata ile ya left, barabara ya kwanza, ya pili, ya tatu ndiyo inaenda nyumbani kwake, ifuate itakuongoza kwa ngetini," akamwelekeza.

Colbas hakusubiri amalizie, alikanyaga klachi akatia gia, akaachia breki na kukanyaga mafuta ngoma ikaondoka. Kama alivyoelekezwa akawasili katika njia hiyo aliyoambiwa lakini hakusimama, akapita kwa mwendo wa taratibu na kuelekea mbele kidogo. Baada ya wigo mkubwa wa shamba la Zuganji, Colbas alifika katika shamba lingine lililotelekezwa, lango lake lilikuwa limefungwa kwa mbao zilizogongewa misumari ya muda mrefu na kuongezewa kufuli chakavu.

Akaingiza gari lake kwa ndani kidogo, akateremka na kuutazama ule mlango.

Akachukua moja ya funguo zake makini na alipocheza na kufuli lile chakavu halikusita kumwitikia. Akababazua zile mbao, zikaachia bila ubishi. Akasukuma taratibu na lile lango likajiachia kisha akarudi garini na kuliingiza ndani, akalificha katika ghala kubwa lililokuwa katika shamba hilo. Akateremka na kasha lake mkononi, akazunguka nyuma huku mkono mmoja ukiwa na bastola tayari kwa lolote. Hatua kadhaa zikamfikisha upande wa nyuma.

"We nani? Shida yako ni gani huku?" akashtushwa na sauti nyuma yake, alipogeuka akajikuta anatazamwa na mtutu wa rifle CZ MODEL "457".


"Weka mikono juu!" akaamriwa. Naye akatii. Akiwa anaiachia bastola yake ifike chini, kwa haraka akainua mguu na kuipiga teke ile bunduki ya yule mtu. Ikamponyoka na kabla hajakaa sawa, Colbas alimtupia teke moja matata lililotua shavuni na kumpeleka chini. Akaiwahi bastola yake na kumtandika risasi ya mbavu.

"Aaaaah… aaaaaah!" yule jamaa aliyekuwa akilinda ghala hilo akaugulia kwa maumivu. Colbas hakuongea kitu, akamtazama na kumnyoshea bastola.

"Nani anaishi katika shamba hilo la pili?" akauliza.

"Kumeil, a-na-i-twa Kumeil," akajibu huku bado maumivu yakimnyanyasa. Risasi ya pili ikamzamisha katika lindi la usingizi mzito wa mauti.

"Sleep well," akamwambia huku yeye akitoka eneo hilo. Pembeni mwa ghala hilo kulikuwa na mnara wa chuma ambao juu yake ulikuwa na kibanda kidogo. Colbas alijua wazi kuwa katika kibanda hicho lazima ndipo mlinzi alipokaa na kuangalia lindo lake.




Hakujiuliza mara mbili, alizikwea ngazi mpaka juu, akaingia ndani ya kibanda hicho na kuvuta kijikiti kidogo, akatulia tuli. Kila mara usingizi ulikuwa ukimnyemelea lakini alihakikisha anapigana nao vikali ili abakie macho atimize kazi yake.

Saa kumi na mbili asubuhi, alisikia muungurumo wa gari kwa mbali, akainuka na kujiweka sawa, akatupa jicho kwa darubini yake yenye nguvu, na kuliona hilo gari likiingia kwenye lango la Kumeil mpaka katika eneo lililoonekana wazi kuwa ni maegesho.

Pale alimuona Zuganji Kumeil akimpokea mwenyeji wake, alipenda kusikia wanaongea nini lakini ilikuwa ngumu kutokana na umbali walipo. Kisha aliwaona wakiingia ndani ya jumba hilo. Alipotazama saa ilikuwa ni saa kumi na mbili na dakika ishirini. Alipoinua macho yake

watu wale walikuwa tayari wamemezwa na jumba lile. Tukio kama lile lilifanyika mara tano hivi na zote hizo Colbas alikuwa akizishuhudia kupitia pale juu alipokuwa ameketi.

Kijua cha asubuhi kilianza kupendezesha eneo hilo, na kijana huyo akafikiri nini cha kufanya ili aweze kutimiza kazi ya bosi wake.

*** *** ***

"Haya mambo yameanza lini? Kila mmoja wetu ana ulinzi wa kutosha inakuwaje Patrick auawe kijinga hivi?" Zunganji akauliza na jopo lote likabaki kimya.

"Kwa kweli hata sisi tumeshtuka, lakini kutoka katika jicho letu inasemekana amedunguliwa," mjumbe mmoja akasema.

"Ndiyo amedunguliwa… lakini nani tumhisi? Mbona hatuna adui na kundi letu?" mjumbe mwingine akaongeza swali.

Ukimya ukatawala kwa nukta za kutosha, hakuna aliyekuwa na jibu kwa wakati huo.
Mmoja kati yao aliyekuwa amevaa suti nyekundu, akasimama na kuzungusha macho yake kwa kila mmoja, kisha akajikohoza kidogo na kufungua kinywa akasema.

"Hatumjui adui?" akauliza, "kama hatumjui basi atakuwa ni mmoja wetu, kwa maana ukiwa humjui adui, basi ujue yuko ndani yako. Nitaondoka hapa leo hii kuelekea London, kule nitakutana na wakubwa wote ili tulijadili pamoja. Hii siyo kawaida kabisa… kumbukeni kuwa Patrick Njuwe alikuwa na dhamana kubwa sana na mradi wetu mpya, na ni nani raia wa nje anayejua juu ya hili? Hata miongoni mwetu kanda na kanda hatujui nini mwingine anafanya, kuna usalama? Hatuwezi kufumba macho bora angekufa mwingine lakini si Njuwe kwa sababu mkononi mwake alikuwa ameshika lulu, funguo ambayo sijui tutafanyaje kuipata!" Hakuna mjumbe aliyeongea kwa maana mara tu akiongea mkubwa huyu basi ninyi wengine hamna budi kukaa kimya. "Tutamfanyia mazishi kama desturi yetu, lakini jibu nitatoa nikitoka London" alipomaliza kusema hayo, akainua mikono juu na alipoishusha kila mjumbe alitoka katika chumba kile kilichojawa mwanga mwekundu tu na kukifanya kiwe kama kimejaa damu.

*** *** ***

Kutoka juu ya kile kidungu, Colbas alishuhudia wale jamaa walivyokuwa wakiondoka katika himaya ya Kumeil. Alipohakikisha kuwa hakuna aliyebaki baada ya kuhesabu yale magari ambayo idadi ya kuondoka ilikuwa sawa na ile ya kufika. Akachukua darubini yake yenye nguvu na kulichunguza jumba hilo. Colbas aliona vijana waliokuwa makini kabisa katika kona mbalimbali za jumba hilo, kwenye lango kuu na hata kwenye baadhi ya kona ambazo labda angeweza kupitia ili kutimiza azma yake. Kichwa kilimuuma kwa jinsi gani ataweza kukamilisha kazi aliyopewa.

Dakika moja baadaye akapata wazo. Akateremka haraka kutoka katika lile dungu na kubeba mkoba wake huku akijua wazi kulitumia tena lile gari kungeweza kumuweka matatani kwa kuwa vyombo vya usalama lazima vitakuwa vinalisaka. Akatoka nje ya lango lile chakavu, akavuta hatua mpaka barabarani na kuanza kuelekea kule ambako alilipita jumba la Kumeil.

Akiwa njiani nyuma yake akaliona gari la kizamani aina ya Peugeot pick up likija upande huo, akalisimamisha.

"Nikusaidie nini?" yule bwana mwenye gari akauliza.

"Nataka nifike kwa Zuganji, mimi ni mgeni wake, lakini sipafahamu," akajibu.

Yule mtu mzima, ndani ya gari lile, akashtuka kidogo, akamtazama kijana huyo aliyevalia nadhifu kabisa.

"Panda!" akamwambia huku akifungua mlango.

"Na una bahati sana, pale huwa hapaingiliki kirahisi, mimi huwa nasambaza maziwa na ninaingia mara nyingi Kadiri ninavyotaka," yule mzee akasema.

"Atakuwa amenisubiri sana, maana nilipotea njia kidogo, ni mara yangu ya kwanza nafika huku," Colbas akajieleza. Muda mfupi baadae wakawa tayari mbele ya lango kubwa la kuingia katika jumba hilo. Kijana mmoja aliyevalia sare ya ulinzi akalisogelea.

**Itaendelea toleo lijalo…**

**Kitabu cha CRONOC 7—chapa ya pili kitakuwa madukani mwezi wa November, 2023.**

**Weka oda yako sasa kwa kutuandikia whatsapp 0766974865.**

**Na ukipenda kulipia kabisa waweza fanya hivyo kwa kutuma pesa '12,000/=' kwenda Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI kisha tutumie meseji ya muamala wako kwa whatsapp hiyo hapo juu.**

# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (2)

Walipomaliza kukutana wote kila mmoja alichukua mizigo yake na kuondoka wote eneo lile wakiongozwa na kiongozi wao wakielekea kule walikotokea. Alibaba aliendelea kukaa juu ya ule mti huku akiangalia safari ya wale wezi wanapoondoka. Akaona asubiri mpaka wapotee kabisa kwa maana asije mmoja akarudi na kumkuta mahali pale.


Walipopotea kabisa mbele ya macho yake Alibaba akashuka kutoka mtini na kwenda mpaka pale kwenye lile doa kisha akajisemea mwenyewe "nitajaribu kutamka maneno yale ya ajabu nione kama kwa kutamka kwangu lile lango litafunguka na kufunga" kisha akasema kwa kelele yale maneno "Funguka, Sesame!!" alipomaliza tu kutamka mara lango likafunguka, kisha akaingia ndani yake.

Akaona pango kubwa lenye kuba likiwa na urefu upatao kadiri ya urefu wa mtu aliekuwa mrefu zaidi duniani, pango lile lilikuwa limezungukwa na mawe na lilikuwa likipitisha mwanga kupitia vitundu vidogovidogo vilivyokuwa katika pango lile na kushangazwa alipoona limejaa kila aina ya bidhaa mle ndani na kumerundikwa kutoka chini mpaka juu rundo la mizigo ya hariri na nguo nzuri zilizotiwa nakshi na matuta juu ya matuta ya makapet na mazulia yenye rangi tofauti na pia aliona sarafu za dhahabu na fedha zikiwa nyingine zimezagaa chini na nyingine zikiwa ndani ya mifuko. Kwa kuona wingi wa mali hizi Alibaba alijifikiria moyoni kuwa sio kwa miaka michache tu, hii itakuwa ni karne na karne wezi wanapora mali za watu na kuja kuzificha humu.

"Hazina nyingi kiasi gani hiki!!" alisema Alibaba. 'na sasa nimezipata' alifikiri kidogo. 'wezi hawa hawawezi kukaa na mali yote hii. Lazima nichukue kiasi cha dhahabu nikajiwekee mwenyewe nyumbani.'

Alisema tena yale maneno "Fungukaa sesmiiii" na lango likafunguka, kisha akenda kuwachukua punda wake watatu aliokuwa amewaficha vichakani.

"Leo ninawapa habari njeeema" aliwaambia punda wake. "leo mtabeba dhahabu na sio kuni kama



mlivyozoea kila siku. Aliwachukua punda wake mpaka karibu na lile pango na kuwaacha nje kasha yeye akaingia tena ndani. "Punda watatu na makapu sita" Alisema alibaba, "Nitajaza makapu yote haya sita dhahabu". Alibaba alichukua makapu yale sita na kujaza kila aina ya dhahabu zilizopo ndani ya lile pango kisha akachukua baadhi ya kuni chache tu kuziweka juu ya kila kapu ili kuzificha zile dhahabu ndani ya kapu zisionekane na watu akiwa njiani, kisha akatoka na kusimama mbele ya lile pango kwa nje na kusema "Fungaaaa Sesmiii!!!" lile pango likajifunga kwa sauti kubwa, Alibaba alitabasamu na kuondoka kuelekea mjini.

Alibaba hakuelekea sokoni kama kawaida yake siku zote, badala yake aliwaongoza punda wake mpaka nyumbani kwake. Aliwapeleka mpaka kwenye kibanda chao na kufunga mlango, kisha akatoa zile kuni chache alizoweka juu ya kapu na kubakia na kapu zake sita zikiwa zimejaa dhahabu.

Alisubiri mpaka giza lilipoingia. Hakutaka mtu yeyote aone hazina ile. Alizichukua kutoka kwenye banda la punda wake na kuzipeleka mpaka ndani kwake kisha akazimimina zote chini fungu moja. Akamuita mke wake kutoka jikoni.

"Angalia!" alisema Alibaba kwa furaha. "sisi ni matajiri sasa mke wangu!, sitafanya tena kazi ya kukata kuni!, tutaweza kula vyakula vizuri vizuri sasa na kuvaa mavazi mazuri!"


Mke wa Alibaba alipoziona zile dhahabu, alishangaa sana. "sijawahi kuona dhahabu nyingi kiasi hiki!" alisema kwa mshangao huku akipepesa macho. 'lakini Kassim ndiye tajiri, na sio wewe!, umezipata wapi hizi? Au umeziiba? .


Basi Alibaba alimpa stori nzima juu ya wale watu 40 na maajabu ya lile pango na mali zilizopo mle ndani.

"Umeona sasa!" Alisema alibaba "kwahiyo nimeziiba, lakini nimeziiba kutoka kwa wezi hivyo hakuna tatizo lolote.

***Nini kitaendelea? Usikose toleo lijalo.***




**VITABU:**

**Jipatie vitabu pendwa vya riwaya tamu za kijasusi. MPATANISHI na HARUFU YA KIFO kutoka Jamvi la Simulizi. Vilivyoandikwa na mwandishi wako wa siku zote ambaye hana maneno mengi ila kalamu yake itakuonesha ubora wake.**

**Wahi sasa katika sehemu elekezwa ili ujipatie chako.**

**MPATANISHI—12,000/= na HARUFU YA KIFO—12,000/=**

**Aidha tunauza nakala laini ya vitabu mbalimbali vya riwaya za kijasusi. Usiwe mpweke, fanya uwezalo ukamate nakala yako.**









# SHUBAKA LA VITABU

**Katika toleo hili la 23, safu ya Shubaka la Vitabu inakuletea mazungumzo mafupi ambayo jarida hili limeyafanya na muasisi wa shirika lisilo la kiserikali la KITABU MAISHA. Ungana nasi kujua nini kilizungumzwa.**

**KITABU MAISHA, Asasi ya Kiraia Iliyojipanga Kuleta Mapinduzi ya Usomaji Tanzania**

**Na. Mwandishi wetu.**
Tunajua kwamba katika nchi yetu kuna mashirika mengi ambayo yamewekeza katika elimu kwa namna tofauti. Mashirika haya ambayo ni ya Kimataifa na ya kitaifa yamejikita miaka na miaka katika kusaidiana na serikali chini ya wizara husika kukuza elimu na kuboresha miundo mbinu anuai ya kielimu.

Asasi ya Kitabu Maisha, chini ya Mkurugenzi na Muasisi, Ndugu Richard Mwambe, nayo imejitokeza katika Nyanja hiyo lakini kwa mtindo wa aina yake. Yeye mwenyewe anatueleza kwa kifupi.

Kwanini Kitabu Maisha?
Ni Kitabu Maisha kwa sababu lengo letu kuu ni kuifanya jamii hususan wanafunzi mashuleni wawe na uwezo wa kukifanya kitabu kuwa maisha yao. Naweza nisieleweke hapo, lakini kwa maana nyepesi ni kwamba, mtu aweze kuyatafsiri yale mazuri ya kwenye vitabu kuwa maisha yake.

Kitabu Maisha ni Asasi ya kiraia iliyosajiriwa chini ya sheri ya mashirika yasiyo ya kiserikali ya mwaka 2002, kwa namba 00NGO/R/4382, mwaka huu wa 2023 mwezi Februari. Kwa sasa ofisi ya shirika hili ipo Iringa na imeanza taratibu kufanya kazi zake katika mkoa huo.
Tunataka tuzifikie shule zote za Sekondari na Msingi kwa program tofauti zenye lengo moja tu la kuwafundisha umuhimu wa kusoma vitabu na faida zake pamoja na kuanzisha mashubaka ya vitabu katika shule hizo hasa za sekondari. Kwa kuwa tumesajiriwa kufanya huduma yetu katika Tanzania Bara, tutajitahidi kadiri ya uwezo wetu kutekeleza. Mpango huu utatekelezwa katika miaka kumi kwanza.

Bado, mpaka sasa hatuna ufadhili wowote; uwe wa ndani au wa nje lakini ni matumaini yetu kuwa utapatikana tu. Mpango wetu ni kwamba wafadhili wa kwanza kabisa wawe rafiki zetu wa hapa nchini. Kama kila rafiki akitupatia kitabu kimoja au zaidi, naamini tutapiga hatua.
Kuhusu aina ya vitabu tunayoihitaji kwa sasa, kwanza ni vitabu vya riwaya za Kiswahili. Unajua katika vitabu hivi kuna mafunzo mengi sana mazuri ambayo yanaweza kumjenga mwanafunzi kuwa mtu bora. Angalisho ni kwamba si kila kitabu cha riwaya tutakitumia bali tutavichagua vile ambavyo kamati maalum itaona vinafaa. Pili ni vitabu vya mafunzo mbalimbali kama ujasiriamali, elimu za fedha, tafiti mbalimbali nk. Tunahitaji msomaji apanuke kimaarifa na ajijue wapi yeye alipo. Hivyo basi ufadhili wa kwanza tunaouhitaji ni vitabu.

Ufadhili wa pili tunaouhitaji ni wa kifedha au vitu. Katika program yetu hii tunahitaji kabati moja kwa kila shule tutakayokuwa na program nayo. Kabati kwa ajili ya kuhifadhi vitabu. Hivyo mtu anaweza kutupatia pesa ili sisi tutengeneze kabati au akatutengenezea kabati kadiri ya mahitaji yetu. Tunahitaji pia Desktop Computer kwa matumizi ya ofisi, rim papers na vifaa vingine kama note books, kalamu, hivi kwa ajili ya vijana wetu.

Mpaka sasa tumepata Laptop Moja tuliyofadhiliwa na mmoja wa marafiki hapa Iringa na tumeahidiwa kupata meza moja ya ofisi kutoka rafiki yetu mwingine.

Hivyo hata wewe unayesoma makala hii unaweza kuwasiliana nasi kutuunga mkono katika hili. Unaweza kutununulia kitabu/vitabu, pesa taslimu hata Tsh 1000 kwetu ina thamani kubwa kwa sasa na vyote ambavyo tumeorodhesha.

Hivi karibuni tutatoa kadi kwa ajili ya fundraising ya vitu mbalimbali. Asante

**Kwa yeyote anayeguswa na anayetaka kutuchangia chochote anaweza kuwasiliana nasi kwa:**

**Simu: 0734 550 514**
**Whatsapp: 0734 550 514**
**Kama unataka kutuma kiasi cha pesa, kwa sasa tunatumia Mpesa Lipa Namba 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Karibuni sana.**

# KITABU NILICHOSOMA

Jina la kitabu:
**ISHI NDOTO YAKO**

Jina la mwandishi: **JOEL ARTHUR NANAUKA**
Jina la msomaji:
**LEAH ZABLON SIARA**


Arusha, Tanzania
Katika kitabu hiki chenye kujaa maarifa ya kila namna yenye manufaa, nimejifunza mengi sana mazuri ya kujenga. Lakini Kwa uchache ni haya hapa

✓ Ili niweze kufanikiwa kufikia ndoto yangu lazima niweke maamuzi ya kufanya jambo na kulitimiza kwa wakati, katika wazo lolote la kuifikia ndoto yangu lazima nichukue hatua haraka na kulifanyia kazi wazo hilo bila kughairi kwani inawezekana wenzako wenye wazo kama langu wakanipita bila kujua.

✓ Kwenye maisha nisikubali changamoto yoyote inishinde Wala inikatishe tamaa bali nitafute mbinu za kuishinda hiyo changamoto ( I must get bigger than my challenge).

✓ Lakini pia nimejifunza kuwa wakati ninafanya jambo lolote lile lazima niwe na subira na uvumilivu Ili nione matunda yake kwanza, nisiwe mtu wa kufanya jambo na kuliachia njiani na kuanza lingine kabla ya kuona mafanikio ya jambo moja. Mwandishi wametumia msemo huu, " Usiwe mfukua mbegu kabla ya kuota"

✓Ninapotafuta njia ya kufikia ndoto yangu nijaribu kuwa chini ya uangalizi wa mtu fulani ambaye tayari amenitangulia katika njia hiyo Ili aweze kuniongoza vyema




✓ Katika kutafuta mafanikio lazima niweke malengo na kuyapa vipaumbele yale ya muhimu hasa katika matumizi ya pesa na muda , Lakini pia niwe mwajibikaji na niweke mikakati nakuifuatilia Kwa karibu ili kutimiza malengo hayo.

✓ Nimejifunza kuwa hali yangu ya maisha ya leo haiwezi kuniamulia kesho yangu, ninachotakiwa ni kufanya maamuzi sahihi ya kile ninachokitaka na kufanya kazi kwa bidii bila kujali watu watasema nini kwani mafanikio yangu yapo mikononi mwangu.

✓Pia nimejifunza kuwa ninapotaka kufanya jambo fulani niondoe HOFU, maana hofu inaweza kunikwamisha katika kuyafikia mafanikio, yaani shauku yangu ya kufanikiwa iwe kubwa kuliko hofu na pia kutokubali kushindwa bali nikiona nimeshindwa nitafute maarifa zaidi na kujaribu tena mpaka nifanikiwe.

Haya ni machache kati ya mengi niliyoweza kujifunza katika kitabu hiki nashukuru sana kwa maarifa haya kutoka "Anna Mbise Mobile Library niliweza kupokea kitabu na kukisoma na kuwashirikisha wanachama wengine wa maktaba hii yale niliyojifunza.

---

Je; na wewe unapenda kusoma kitabu na kutuandikia ulichojifunza?

Je; ungependa kuwa mwanachama wa Anna Mbise Mobile Library? Kama NDIYO basi tuma ujumbe

“NIAZIME KITABU” kwenye facebook Messenger nawe utapewa utaratibu.

Anna Meleiya Mbise (Faebook, Twitter, Linkedn na Tik Tok)
Email: annambise@gmail.com
+255 766 069962

Anna Mbise
Mobile Library

# Tangazo










---

www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com